



TIST HABARI MOTOMOTO JULY 2024

www.tist.org. Email: info@tist.org Tel. +255784-537720



Photo 1: Kisokwe Cluster Meeting which was held in July 2024.

In this newsletter, we are going to have three articles;

- (i) The TIST Best Practice of Preparing Raised Seedbeds
- (ii) Making your Small Group eligible for Pre-payments
- (iii) TIST Pre-Payments Are Ready

TIST HABARI MOTO MOTO

(i) The TIST Best Practice of Preparing Raised Seedbeds

TIST Small Group Farmers we are encouraged to try raised beds because they improve the survival of the trees. Traditional systems of arranging pots on the ground can produce few seedlings with weak roots. This is because the roots coil up and at transplanting, because of roots being weak may not establish well in the ground. To avoid this, it is recommended to establish seedlings in open bottom tubes placed on raised beds.

A raised bed can easily be made from a wooden frame and wire mesh (see photo) or wooden slats. These allow automatic root pruning because when the roots get to the container bottom, they naturally drop off (called air root pruning). This means that roots do not get injured through normal root pruning methods. The roots then tend to strengthen without growing further.

This produces a healthy root system, and the seedling has higher chances to establish faster in the field. It also eliminates the need for labour to do root pruning, a practice that is often forgotten or done too late, causing serious damage to the roots. Weed control under the raised beds is also easier, and the raised beds have excellent drainage, so roots are less likely to be damaged by heavy rain. Seedlings grown in raised beds may be fragile in transport, so be careful when moving seedlings for transplanting.

If your Small Group has already practiced raised beds; please share your results with your Cluster members and other TIST Farmers! We would love to learn from your Small Group!



Photo 2: An example of a Raised Seedbed. Best Practice from one of the groups in Kenya

TIST HABARI MOTO MOTO

(ii) Making your Small Group eligible for Pre-payments

During your Cluster meeting, please review the requirements for your Small Group to receive their Pre-payment. Please help one another to understand them. They are important in our TIST activities and in achieving big results. When the Small Group's information is accurate, and the Small Group is eligible for payment, TIST earns trust and a good reputation in the Carbon Market, which increases the value of TIST carbon. If your Small Group does not complete these requirements, your carbon may not be able to be sold in the Carbon Market.

Your Small Group should meet the following requirements to qualify for payments.

- There should be 6 to 12 members in your Small Group from at least three different families.
 - Each Small Group member must be willing to follow the TIST Values.
 - Each active grove in the group should have been quantified in the last 18 months.
 - Each Small Group member is required to sign the Greenhouse Gas contract.
 - Each Small Group should have at least 500 trees in the group
 - Each active grove should have a good boundary of their land taken.
 - Groves should not count trees that were planted before the members were involved in TIST as TIST trees.
- Baseline information must be collected and accurate.
 - Each Small Group member should provide information on whether any activities were displaced or moved on their farms, like buildings or farming activities.
 - Small Group members should say if their land has been forested anytime since 1990.
 - Groves should not have any Eucalyptus trees counted for TIST planted after 2022.
 - Each Small Group member should review and sign each voucher.
 - Each Small Group member signing the voucher should be included in the GHG contract.

If your group has not met each requirement above or is unsure if you have met each requirement, please work with your Cluster Servant. Your Cluster Servant is responsible for reviewing these requirements and updating our information in the computer database.

(iii) TIST Pre-Payments Are Ready

We are glad many Small Groups continue to abide by the Greenhouse Gas contract and the TIST values.

The GhG contract, among other requirements, asks the Small Groups to keep their trees alive for a minimum 30 years. This is necessary to make carbon business Sustainable and profitable for the long-term.

We however, have Small Groups that have not fully understood the importance of keeping their trees alive. They cut their trees without considering the harmful effects their actions have on other farmers.

TIST Tonnes continues to get good buyers in the market. Our buyers get confidence from many farmers who continue to keep their trees alive and do other activities (co-benefits) in their farms. In the carbon business, farmers who are producers of the carbon tonnes, and the carbon buyers are both protected by rules governing the carbon market.

As carbon producers earn revenue from carbon tonnes sales, carbon buyers get assurance that trees will be kept alive and no carbon will be lost through harvesting.

Therefore, during payments, TIST quickly pays Small Groups that are in good standing.

These Pre-payments intends to enhance the process of payments by making it easier and quicker. The payments will be in two (2) major phases

First phase

Small Groups that have met minimum criteria for pre-payment eligibility will be paid during the first phase.

Like in previous Pre-payments, Eligible Small Groups are required to do the following in order to make payments efficient, transparent and credible.

1. Upon receiving payment receipt (voucher), all members of the Small Group should append their signatures, ID numbers and their full Names.
2. Small Groups should have their trusted Mobile Money Custodian who will receive payments on their behalf. Custodians should provide full names, ID numbers and Phone numbers that will be used to receive money.

Second Phase

The second phase will require extra work by Small Groups working together with Cluster Servants. Some of these Groups are missing critical information that is needed for them to be paid, because each Small Group has unique circumstances.

1. Small Groups with less than 6 members.

Your Small Group is allowed to add new members and sign new GhG.

Your Cluster Servant will provide you with a New GhG Contract.

Please Note: New members should come with new trees. Old trees are not allowed. They are considered as Baseline Trees.

2. Small Groups with inheritance issues

If one of the members of your Small Group has shared his land with the beneficiaries, those beneficiaries are required to commit with a letter that they are not going to harvest. This letter should be clear with full names, ID numbers, phone numbers and signatures.

3. GhG not tallying with Registration

Some Small Groups have issues with people who registered being different from people who signed GhG contract or who get quantified.

Your Cluster Servant will work with you to fix this problem

4. Missing Baseline information

Carbon market rules and regulations require every Grove to have complete baseline information. Some Small Groups are missing this information. Please talk to your Cluster Servant and check if your Small Group is Okay or it need to complete Baseline information.

5. Bad Tracks

When Quantifiers visit your farm, the carbon rules require they mark track boundaries of your Grove. This is because, only Trees within the track boundary count for carbon tonnes. Sometimes, this track is not complete or it was taken badly.

It is important you talk to your Cluster Servants to check if your Groves are in good shape. If they have a problem, please ask your Cluster Servant to fix them.

6. Small Groups that have added members

Some Small Groups have added new members. These new members have not signed the GhG contract. It is a requirement of the carbon market rules that members participating in carbon credits have a contract with project companies such as CAAC.

In order to accomplish this, talk to your Cluster Servants if you have added any new members, and CS will issue you with a new contract.

Please note: It is important that old members of your Small Group give consent to admission of new members.

New members should always join with new trees (1 year old).

TIST HABARI MOTO MOTO

TIST Values

As TIST Family we have our Values which most of TIST Small Groups know and practice. We always reflect on these Values and to ensure that we all are truly living by them. The success of TIST is based on the integrity and effort of individual members within TIST. What we can achieve depends on each of us following these Values;

- (i) *We are Honest*
- (ii) *We are Accurate*
- (iii) *We are Transparent*
- (iv) *We are Servants to each other*
- (v) *We are Mutually Accountable to Each Other and*
- (vi) *We create Low Budget/ cost, yet we achieve Big Results.*

INTRODUCTION OF CLUSTER SERVANT

In the pictures is a **Cluster Servant JOSHUA JAMES MAZENGO** from Mwanakianga, Mpwapwa district. He is a Farmer from Mazingira Group with TIST number 2003TZ145. He joined TIST in the year 2003.

Joshua serves three (3) Clusters: Kisokwe, Idilo and Mazae Clusters. Experienced in quantification (tree counting), recruitment of new Small Groups, data entry into Pendragon and Conservation Farming. Also he provides TIST seminars to the Small Groups across the whole TIST Program in Tanzania.

If you have any questions, or you need help on how to join the TIST Program, you may contact him through;



Photo 3: Joshua James, a Cluster Servant from Mpwapwa district.



TIST HABARI MOTOMOTO JULAI 2024

www.tist.org. Email: info@tist.org Tel. +255784-537720



Picha 1: Mkutano wa Klasta ya Kisokwe Mpwapwa, uliofanyika mwezi Julai 2024

Katika jarida hili, tutakuwa na makala tatu:

- (i) **Mbinu Bora ya TIST ya Kutayarisha Vichanja/Vitalu vya Mbegu vya juu**
 - (ii) **Namna ya Kufanya ili Kikundi chako Kidogo kistahiki kwa Malipo ya Mapema**
 - (iii) **Malipo ya Awali ya TIST Yako Tayari**
-

(i)Mbinu Bora ya TIST ya Kutayarisha Vichanja vya Mbegu

Wakulima wa Vikundi Vidogo Vidogo vya TIST tunahimizwa kujaribu kutumia vichanja/vitalu vya juu kwa sababu vinaboresha maisha ya miche. Utaratibu wa kuotesha miche kwa kupanga makopo au viriba chini inaweza kutoa matokeo ya miche michache na yenye mizizi dhaifu. Hii ni kwa sababu mizizi hujikunja wakati wa kupandikiza, kwa sababu ya mizizi kuwa dhaifu hivyo inaweza isisitawi vizuri ardhini. Ili kuepuka hili, inashauriwa kuanzisha miche kwenye viriba vilivyo wazi chini vilivyowekwa kwenye vichanja/vitalu vya juu.

Kichanja/Kitalu cha juu kinaweza kutengenezwa kwa urahisi kwa kutumia mbao na waya (tazama picha). Kitendo hiki cha kuweka miche kwenye kichanja huruhusu upogoaji wa mizizi wa moja kwa moja kwa sababu mizizi inapofika chini ya viriba hutokeza (hii inaitwa upogoaji wa hewani). Hii ina maana kwamba mizizi haijeruhiwi kwa njia ya kawaida ya kupogoa mizizi. Kisha mizizi huwa inaimarika bila kurefuka zaidi.

Kitendo hiki hufanya mfumo wa mizizi kuwa wenye afya, na miche inakuwa na nafasi kubwa ya kustawi vizuri shambani. Pia huondoa usumbufu wa kupogoa mizizi, kazi ambayo mara nyingi husahaulika au hufanywa kwa kuchelewa, na kusababisha uharibifu mkubwa kwa mizizi. Udhibiti wa magugu chini ya vitalu vya juu pia ni rahisi na vinapitisha maji kwa urahisi, hivyo kuna uwezekano mdogo wa mizizi kuharibiwa na mvua kubwa. Miche iliyopandwa kwenye vitalu vya juu inahitaji uangalifu wakati wa usafirishaji, hivyo uwe mwangalifu wakati wa kuhamisha miche kwa ajili ya kupandikiza.



Picha 2: Mfano wa Kitalu cha juu. Mbinu Bora kutoka kwa moja ya vikundi nchini Kenya.

TIST HABARI MOTO MOTO

(ii) Namna ya Kufanya ili Kikundi chako Kidogo kistahiki kwa Malipo ya Awali

Wakati wa mkutano wa Klasta, tafadhali tusaaidiane kuelewa na kukagua mahitaji ya Kikundi chako Kidogo ili kiweze kustahiki kupokea Malipo Mapema. Ni muhimu katika shughuli zetu za TIST na katika kufikia matokeo makubwa. Maelezo ya Kikundi Kidogo yanapokuwa sahihi, na Kikundi Kidogo kikiwa na sifa za kustahiki malipo, TIST inapata sifa nzuri na kuamini katika Soko la Kaboni, jambo ambalo huongeza thamani ya kaboni kwa TIST. Ikiwa Kikundi chako Kidogo hakitakamilisha mahitaji haya, kaboni yako inaweza isiweze kuuzwa kwenye Soko.

Kikundi chako Kidogo kinapaswa kukidhi mahitaji yafuatayo ili kupata malipo.

- Kikundi chako Kidogo kinapaswa kuwa na wanachama 6 hadi 12 kutoka angalau familia tatu tofauti.
- Kila mwanakikundi Kidogo lazima awe tayari kufuata Maadili ya TIST.
- Kila mwanachama wa Kikundi Kidogo anatakiwa kutia saini mkataba wa Gesi ya Kaboni.
- Kila shamba hai katika kikundi linapaswa kuwa limehesabiwa katika muda wa miezi 18 iliyopita.
- Kila Kikundi kinapaswa kuwa na angalau miti 500 ya kikundi
- Miti iliyopandwa kabla ya wana Kikundi Kidogo kujiunga na TIST haipaswi kuhesabiwa kama miti ya TIST.

- Taarifa za awali za kila shamba (Baseline) lazima zikusanywe kwa usahihi.

o Kila Mwanakikundi Kidogo anapaswa kutoa taarifa kama shughuli zozote zilihamishwa au kuhamishwa kwenye mashamba yao, kama vile majengo au shughuli za kilimo.

o Kila mwanachama wa Kikundi Kidogo anapaswa kusema kama ardhi yao imekuwa na misitu wakati wowote tangu 1990.

- Kila shamba linaloendelea linapaswa kuwa na mipaka mizuri ili kudhibiti ardhi yao kuchukuliwa.

● Miti iliyopandwa kabla ya wana Kikundi Kidogo kujiunga na TIST haipaswi kuhesabiwa kama miti ya TIST.

● Shamba la miti halipaswi kuwa na miti ya Mikaratusi iliyopandwa baada ya mwaka 2022.

● Kila mwanachama wa Kikundi Kidogo anapaswa kukagua na kutia sahihi kila vocha.

● Kila mwanachama wa Kikundi Kidogo anayetia saini vocha lazima ajumuishwe kwenye mkataba wa GHG.

Ikiwa kikundi chako hakijatimiza mahitaji yote hapo juu au hakina uhakika kama kimetimiza kila hitaji, tafadhali shirikiana na Mtumishi wako wa Klasta. Mtumishi wako wa Klasta ana wajibu wa kukagua mahitaji haya na kuingiza taarifa kwenye kompyuta

(iii) Malipo ya Awali ya TIST Yako Tayari

Tunafurahi Vikundi vingi Vidogo vinaendelea kutii mkataba wa Gesi ya Kaboni na maadili ya TIST.

Mkataba wa GhG, miongoni mwa mahitaji mengine, unavitaka Vikundi Vidogo kutunza miti yao kwa muda usiopungua miaka 30. Hii ni muhimu ili kufanya biashara ya kaboni kuwa endelevu na yenye faida kwa muda mrefu.

Hata hivyo, tuna Vikundi Vidogo ambavyo havijaelewa kikamilifu umuhimu wa kutunza miti yao. Wanakata miti yao bila kuzingatia madhara ya matendo yao kwa wakulima wengine.

Tani za Kaboni za TIST zinaendelea kupata wanunuzi wazuri sokoni. Wanunuzi wetu wanapata imani kutokana na wakulima wengi wanaoendelea kutunza miti yao na kufanya shughuli nyingine (co-benefits) katika mashamba yao. Katika biashara ya kaboni, wakulima ambao ni wazalishaji wa tani za kaboni, na wanunuzi wa kaboni wote wanalindwa na sheria zinazoongoza soko la kaboni.

Wazalishaji wa kaboni wanapopata mapato kutokana na mauzo ya tani za kaboni, wanunuzi wa kaboni hupata hakikisho kwamba miti itahifadhiwa hai na hakuna kaboni itakayopotea kupitia uvunaji. Kwa hivyo, wakati wa malipo, TIST hulipa haraka Vikundi Vidogo vilivy katika hadhi nzuri.

Malipo haya ya awali ya 2023 yanalenga kuimarisha mchakato wa malipo kwa urahisi na haraka. Malipo yatakuwa katika awamu kuu mbili (2):

Awamu ya kwanza

Vikundi Vidogo vilivyokidhi vigezo vya chini zaidi vya kustahiki malipo ya awali vitalipwa katika awamu ya kwanza.

Kama ilivyokuwa katika Malipo ya awali, Vikundi Vidogo Vidogo Vinavyostahiki vinatakiwa kufanya yafuatayo ili kufanya malipo yafanyike kwa ufanisi, uwazi na uaminifu.

1. Baada ya kupokea risiti ya malipo (vocha), wanachama wote wa Kikundi Kidogo wanapaswa kuambatisha saini zao, nambari za vitambulisho na Majina yao kamili.

2. Vikundi Vidogo vinapaswa kuwa na Wakala wao anayeaminika ambaye atapokea malipo kwa niaba yao. Mawakala wanapaswa kutoa majina kamili, nambari za kitambulisho na nambari za simu za mtandao utakaopokea pesa.

TIST HABARI MOTO MOTO

Awamu ya Pili

Awamu ya pili itahitaji kazi ya ziada ya Vikundi Vidogo vinavyofanya kazi pamoja na Watumishi wa Klasta. Baadhi ya Vikundi hivi vinakosa taarifa muhimu zinazohitajika ili walipwe, kwa sababu kila Kikundi Kidogo kina mazingira ya kipekee, tutakuwa tukituma barua mahususi zinazoeleza kile wanachohitaji kutimiza ili kustahili malipo.

*Kazi ya ziada Kikundi chako Kidogo kinaweza kufanya kazi pamoja na Mtumishi wa Klasta kurekebisha *

1. Vikundi vidogo vyenye wanachama wasiozidi 6.

Kikundi chako Kidogo kinaruhusiwa kuongeza wanachama wapya na kusaini mkataba mpya wa GhG.

Mtumishi wako wa Klasta atakupua Mkataba Mpya wa GhG.

Tafadhali Kumbuka: Wanachama wapya wanapaswa kuwa na miti mipya. Miti ya zamani hairuhusiwi na itahesabiwa kama Miti ya awali.

2. Vikundi vidogo vyenye masuala ya mirathi

Ikiwa mmoja wa wanachama wa Kikundi chako Kidogo amegawana ardhi yake na wanufaika, walengwa hao wanatakiwa kutoa maelezo kwa barua kwamba hawatavuna miti. Barua hii iwe wazi na iwe na majina kamili, nambari za kitambulisho, nambari za simu na sahihi.

3. GhG hailingani na Usajili

Baadhi ya Vikundi Vidogo vina matatizo na watu waliojiandikisha kuwa tofauti na watu waliotia saini mkataba wa GhG au wanaohibitishwa. Mtumishi wako wa Klasta atafanya kazi nawe kurekebisha tatizo hili.

4. Taarifa za Awali zinazokosekana

Sheria na kanuni za soko la kaboni zinahitaji kila shamba liwe na taarifa kamili za msingi (awali). Baadhi ya Vikundi Vidogo vinakosa taarifa hizi. Tafadhali zungumza na Mtumishi wa Klasta yako na uangalie kama taarifa za Kikundi chako Kidogo ziko sawa au kinahitaji kukamilisha maelezo ya Msingi.

5. Track Mbaya

Wakadiriaji wanapotembelea shamba lako, sheria za kaboni zinahitaji waweke alama kwenye mipaka ya shamba lako. Hii ni kwa sababu, miti iliyo ndani ya mipaka ya track pekee ndiyo inayohesabiwa kwenye tani za kaboni. Wakati mwingine, track inakuwa hajjakamilika au ilichukuliwa vibaya.

Ni muhimu uzungumze na Watumishi wa Klasta yako ili kuangalia kama Shamba lako liko katika hali nzuri. Iwapo kuna matatizo, tafadhali mwombe Mtumishi wako wa Klasta ayarekebishe.

6. Vikundi vidogo vilivyoongeza wanachama

Baadhi ya Vikundi Vidogo vimeongeza wanachama wapya. Wanachama hawa wapya hawajatia saini mkataba wa GhG. Ni sharti la sheria za soko la kaboni kuwa wanachama wanaoshiriki katika biashara ya kaboni wawe na mkataba na kampuni za mradi kama vile CAAC.

Ili kutimiza hili, zungumza na Watumishi wa Klasta yako ikiwa umeongeza wanachama wowote wapya, na Mtumishi wa Klasta atakupua mkataba mpya. **Tafadhali kumbuka:** Ni muhimu kwamba wanachama wa zamani wa Kikundi chako Kidogo watoe idhini ya kuongeza wanachama wapya. ***Wanachama wapya wanapaswa kujiunga na miti mipya va mwaka mmoja.***

TIST HABARI MOTO MOTO

MAADILI YA TIST

Kama Familia ya TIST tuna Maadili yetu ambayo wengi wa Wanavikundi Vidogo vya TIST wanayajua na kuyatekeleza. Daima tunatafakari juu ya Maadili haya na kuhakikisha kwamba sote tunaishi kulingana nayo. Mafanikio ya TIST yanatokana na uadilifu na juhudi za wanachama binafsi ndani ya TIST. Tunachoweza kufikia inategemea kila mmoja wetu kufuata Maadili haya;

- 1) Sisi ni Waaminifu
- 2) Sisi Tunatoa Taarifa Sahihi
- 3) Sisi ni Wawazi
- 4) Sisi Tunatumikiana
- 5) Sisi ni Wawajibikaji
- 6) Bajeti Ndogo, Matokeo Makubwa

UTAMBULISHO WA MTUMISHI WA KLASTA (CLUSTER SERVANT)

Katika picha ni **Mtumishi wa Klasta JOSHUA JAMES MAZENGO** kutoka Mwanakianga Mpwapwa. Ni Mkulima kutoka Kikundi cha Mazingira kililchopo Igovu chenye namba ya TIST 2003TZ145. Alijiunga na TIST mwaka 2003.

Joshua anatumikia Klasta tatu (3): Kisokwe, Idilo na Mazae. Ana Uzoefu wa kuhesabu miti (Quantification) na kuingiza takwimu kwenye Pendragon. Anatoa mafunzo kwenye Vikundi na kwenye mikutano mbalimbali ya kijamii. Pia anaviunga Vikundi Vidogo Vidogo kwenye Mpango mzima wa TIST nchini Tanzania.

Ikiwa una maswali yoyote, au unahitaji usaidizi jinsi ya kujiunga na Mpango wa TIST, unaweza kuwasiliana naye kupitia 0675059885 au 0742059882



Picha 3: Mtumishi wa Klasta Joshua James Kutoka wilaya ya Mpwapwa